# JOTOARDHI JARIDA

## KAMPUNI YA UENDELEZAJI JOTOARDHI TANZANIA

TOLEO LA NNE, 2025

**MD LAZARO TWANGE WA TANESCO ATUA TGDC,**



**OSAKA EXPO 2025**

**TGDC Yaonesha Ubunifu wa Nishati ya Jotoardhi Katika Wiki ya Nishati Jadidifu 2025**

## JICHO LA MWENYEKITI

KATIKA MUHULA HUU WA MWISHO WA MWAKA WA FEDHA 2024/2025, TUNAPOJITATHMINI NA KUJIPANGA KWA MWAKA UJAO, TUNAYO MENGI YA KUSHEREHEKEA. TUMEPITA KATIKA MILIMA, MABONDE HATA FURAHA CHA MUHIMU VYOTE HIVI VIMETUPA CHACHU YA KUPAMBANA ZAIDI ILI KUFIKIA LENGO LETU KUU YA UPATIKANAJI WA RASILIMALI YA JOTOARDHI. TUMEENDELEA KUIMARISHA JUHUDI ZETU ZA UTAFITI WA MAENEO YA JOTOARDHI NA KUENDELEZA KUSHIRIKIANA NA WADAU MBALIMBALI WA NDANI NA NJE YA NCHI HASA SERIKALI YETU KWA KUHAMASISHA WADAU  KUHUSU FURSA ZA NISHATI JADIDIFU KWA MAENDELEO ENDELEVU YA TAIFA LETU.

JARIDA HILI LINAWALETEA TAARIFA MBALIMBALI KUHUSU MIRADI YETU, USHIRIKI WETU KATIKA MATUKIO YA KITAIFA NA KIMATAIFA, MAFANIKIO YA TIMU YETU, PAMOJA NA MCHANGO WA TGDC KATIKA KUKUZA AJENDA YA NISHATI JADIDIFU NCHINI KATIKA ROBO YA NNE YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. PIA BILA KUSAHAU PONGEZI ZIENDE WASUKUMA GURUDUMU MUHIMU WAFANYAKAZI WA TGDC KWA KAZI KUBWA WANAYOIFANYA KILA SIKU KUHAKIKISHA RASILIMALI YA JOTOARDHI INAPATIKANA  KWA MSHIKAMANO NA USHIRIKIANO THABITI.

TUNAPOFUNGA MWAKA HUU, TUNAANGALIA MBELE YA KAMPUNI YETU KWA JICHO LA MATUMAINI KWA KUONA TANZANIA YETU INAFIKIA LENGO LA MISSION 300 AMBAYO INAHITAJI KAMPUNI YETU ITOE MEGAWATI 130 ZA NISHATI YA JOTOARDHI IFIKAPO MWAKA 2030, TUKIJIVUNIA MSINGI TULIOUWEKA WA MEGAWATI MOJA KWA KILA MTUMISHI NA TUKIWA NA MATARAJIO YA KUONGEZA JUHUDI ZAIDI  KATIKA MWAKA UJAO WA 2025/2026.

ASANTE KWA KUWA SEHEMU YA SAFARI HII YA KULETA MABADILIKO KUPITIA NISHATI SAFI, SALAMA,RAFIKI WA MAZINGIRA NA ENDELEVU.NASISITIZA TUITIZAME MBELE

TUNASTAHILI NISHATI SAFI

**IMEANDALIWA NA;**

MATHEW MWANGOMBA – **MWENYEKITI**
KHADIJA AHMED  -**MHARIRI MKUU**
BOAZ MAZIGO  - **MHARIRI MSAIDIZI**
LEONCE KOMBA - **MSANIFU KURASA**

HOTUBA YA

# BAJETI WIZARA YA NISHATI

APRILI 28, 2025 — BUNGENI, DODOMA






## JOTOARDHI KATIKA BAJETI YA 2025/26

1. Serikali imeamua kuchukua hatua madhubuti za kuwekeza katika vyanzo mbalimbali vya umeme, ikiwa ni pamoja na umeme wa Jotoardhi.

2. Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania, (TGDC), inaendelea na tafiti katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza rasilimali ya Jotoardhi. Hadi sasa, zaidi ya maeneo 50 yamebainika kuwa na rasilimali hiyo.

3. Licha ya kuanza mwaka 2013, tumepiga hatua kubwa. Hivi sasa, mkandarasi yupo eneo la mradi tayari kwa kuchoronga kisima cha kwanza cha utafiti katika eneo la Ngozi.

4. Katika bajeti ya mwaka huu, tumeomba shilingi bilioni 34 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Jotoardhi.





**Prof. Shubi Kaijage**
**Mwenyekiti wa Bodi-TGDC**



**Mha. Mathew Mwangomba**
**Meneja Mkuu-TGDC**

## Serikali Yatilia Mkazo Uwekezaji Katika Jotoardhi, Bajeti Mpya 2025/2026

Katika wasilisho la hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, ameelezea dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwekeza kwenye vyanzo mbalimbali vya uzalishaji umeme, hususan nishati jadidifu ya jotoardhi.

Akizungumza bungeni jijini Dodoma, Mhe. Biteko alieleza kuwa jotoardhi ni miongoni mwa vyanzo vya nishati vinavyopewa kipaumbele katika mpango wa taifa wa kuongeza uzalishaji wa umeme wa uhakika, wa bei nafuu na rafiki kwa mazingira.

Aidha, alitoa pongezi kwa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) kwa hatua kubwa iliyopiga katika kuendeleza miradi ya jotoardhi, hususan mradi wa Ngozi ambao umeendelea kuonyesha mafanikio makubwa katika maandalizi na utekelezaji wake.

Mhe. Biteko alibainisha kuwa kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026, Serikali imeweka mipango mahsusi ya utekelezaji wa miradi ya jotoardhi, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya uchimbaji wa kisima cha kwanza cha uhakiki na kuimarisha miundombinu ya uendelezaji wa miradi hiyo.

# MD Lazaro Twange wa TANESCO Atua TGDC, Asema, Watanzania Wanahitaji Kuuona Umeme wa Jotoardhi Atamani Kuwa Sehemu ya Historia ya Uzalishaji Umeme wa Jotoardhi

TGDC Makao Makuu, Dar es Salaam.
Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Bw. Lazaro Twange amefanya ziara ya kikazi kwa kuitembelea Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) ambayo ni Kampuni Tanzu ya shirika hilo Mei 15, 2025 kwa lengo la kuzifahamu taasisi zilizo chini ya shirika analolisimamia.

Akiongea na Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti pamoja na watumishi akiwa katika ofisi za TGDC makao makuu, MD Twange ameeleza kufurahishwa kwake na wale walioanzisha wazo hadi uwepo wa taasisi hii iliyoanzishwa mwaka 2013 kwa lengo la kuendeleza rasilimali ya jotoardhi nchini ili kuzalisha umeme. Pia, ameipongeza TGDC kwa ujumla kwa utendaji kazi nzuri akitambua kuwa uanzishwaji wa jambo mpaka kuleta matokeo huchukua mda mrefu lakini hatua ni nzuri na kusisitiza kuwa Watanzania wanahitaji umeme.

"ninamshuruku Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuwa mtumishi wa TANESCO na niwapongeze sana walioanzisha wazo mpaka leo tunayo TGDC. Pia niwapongeze wote kuanzia Bodi ya Wakurugenzi mpaka wafanyakazi kwa utekelezaji mzuri wa kazi. Vilevile niwaambie kuwa, Watanzania wanahitaji kuuona umeme wa jotoardhi; hivyo, ninaomba sana tujitahidi , wananchi wauone umeme huu ", alisema MD Twange.

MD Twange alimaliza kwa kusema, "nitafurahi kuwa sehemu ya shuhuda wakati wa upatikanaji wa umeme huu na niko tayari kufanya kazi na kila mmoja wenu, nitawapa ushirikiano na ninafurahi kwamba, kazi nyingi zimefanywa na wazawa. Ninatamani mjue yakwamba, watu wanataka kuridhika na kuridhika kwao ni kuupata umeme wa jotoardhi"







Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TGDC Prof. Shubi Kaijage alimkaribisha na kumpongeza kwa kuteuliwa, lakini pia kwa kufika na kuwasalimu wafanyakazi na kisha kumhakikishia kuwa, maelekezo yaliyotolewa yatafanyiwa kazi na menejimenti inaendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kuleta matokeo.

Awali akitoa maelezo ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ndani ya taasisi, Meneja Mkuu wa Kampuni ya TGDC Mhandisi Mathew Mwangomba alieleza kuwa, TGDC inaamini kuwa, umeme wa jotoardhi utakapozalishwa, Tanzania itakuwa imeondokana na changamoto ya upatikanaji wa umeme kwa kiasi kikubwa kupitia vyanzo msteto na kusema kuwa, ndani ya muda mfupi anaamini watatoa matokeo chanya wakitarajia kuanza kuchimba visima vya uhakiki wa mradi wa Jotoardhi Ngozi kwa lengo la kuzalisha umeme.

Mhandisi Mwangomba aliongeza kuwa, utafutaji wa rasilimali ya jotoardhi unahitaji uwekezaji mkubwa na teknolojia ya hali ya juu, jambo linalopelekea TGDC kuendelea kuomba ushirikiano wa karibu kutoka kwa viongozi wake mbalimbali akiwemo MD Twange ili kuweza kufanikisha azma yake na kuhitimisha kwa kusema, kila mtumishi wa TGDC anadaiwa Megawati 1 ambayo inapatikana kwa kila mmoja kutekeleza jukumu lake na kwamba wafanyakazi wana ari ya kazi na watatoa matokeo.

TGDC ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambayo inamilikiwa na serikali ya Tanzania kwa 100% iliyoundwa tarehe 19 Desemba 2013 kwa lengo la kuendeleza rasilimali ya jotoardhi (geothermal) nchini na kuanza rasmi tarehe 1 Julai, 2014. Kazi yake ni kufanya utafiti, maendeleo, na uendeshaji wa miradi ya nishati ya jotoardhi.

Hadi hivi leo, TGDC imekwisha kuainisha maeneo takribani 52 katika mikoa 16 ya Tanzania bara yenye viashiria vya nishati ya jotoardhi ambavyo vyote kwa pamoja vinakadiriwa kuzalisha Megawati 5000 za umeme na Megawati 15,000 za joto kwa matumizi mengineyo

***"Ninamshuruku Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuwa mtumishi wa TANESCO na niwapongeze sana walioanzisha wazo mpaka leo tunayo TGDC. Pia niwapongeze wote kuanzia Bodi ya Wakurugenzi mpaka wafanyakazi kwa utekelezaji mzuri wa kazi. Vilevile niwaambie kuwa, Watanzania wanahitaji kuuona umeme wa jotoardhi; hivyo, ninaomba sana tujitahidi wananchi wauone umeme huu",***

**MD Twange.**







# OSAKA EXPO 2025

OSAKA, KANSAI, JAPAN





MUNGU AKIPENDA, TUKUTANE MWAKANI

# Waziri wa Maliasili na Utalii Aipongeza TGDC Katika Maonesho ya Osaka, Japan

Osaka, Japan – Juni 2025 — Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), alikutana na Mhandisi Mathew Mwangomba, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Osaka Expo yaliyofanyika nchini Japan.

Katika tukio hilo, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alii-pongeza TGDC kwa juhudi zake endelevu katika kuendeleza nishati ya jotoardhi nchini Tanzania, na alisisitiza kuwa nishati jadidifu hiyo itakuwa kichocheo muhimu cha maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii.

Aidha, kupitia jukwaa la Osaka Expo, Waziri Chana alitumia fursa hiyo kutangaza fursa za utalii wa jotoardhi, ambapo aliwahamasisha wawekezaji na wadau wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta hii mpya inayochipukia, yenye uwezo mkubwa wa kukuza uchumi na kuvutia watalii.

Maonesho ya Osaka Expo yatabaki kuwa jukwaa muhimu kwa Tanzania kutangaza rasilimali zake, fursa za uwekezaji, na miradi ya kimkakati kama jotoardhi, ambayo imelenga kuleta mageuzi katika sekta ya nishati na utalii nchini.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), walipokutana na Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Mathew Mwangomba, Osaka Japan.

# OSAKA EXPO 2025
# MATUKIO KATIKA PICHA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Alishuhudia utiaji saini wa mikataba mbalimbali, Osaka, Japan





# Waziri Mkuu Aalika Wawekezaji wa Kijapani Kuchangamkia Fursa za Jotoardhi Nchini Tanzania

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), alifanya kikao muhimu na Shirikisho la Wafanyabiashara wa Japan (KEIDANREN), ambalo linajumuisha wawekezaji wakubwa na viongozi wa biashara nchini Japan.

Katika kikao hicho, Waziri Mkuu alieleza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizokuwepo nchini Tanzania, huku akisisitiza zaidi sekta ya nishati, hususan nishati ya jotoardhi. Alibainisha kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali za jotoardhi ambazo zinaweza kutumika kuzalisha umeme wa uhakika na wa gharama nafuu kwa ajili ya kukuza viwanda na kuendeleza uchumi endelevu. Kwa upande wa TGDC, kikao hiki kiliwakilishwa na Meneja Mkuu Mha. Mathew Mwangomba.

Waziri Mkuu aliwaalika wawekezaji wa Japan kufika Tanzania na kuchunguza fursa za kuwekeza katika sekta ya jotoardhi, akihimiza ushirikiano kati yao na Serikali kupitia taasisi zake, ikiwemo Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC). Alisisitiza kuwa nishati ya jotoardhi ni fursa ya kimkakati yenye manufaa kwa pande zote mbili—Tanzania na Japan.

Katika kuimarisha ushirikiano huo, TGDC ilisaini Hati ya Makubaliano (MoU) na kampuni ya Toshiba Energy Systems & Solutions Corporation ya Japan, kwa lengo la kuweka msingi wa ushirikiano wa kimkakati katika maendeleo ya nishati ya jotoardhi.

Uwekaji saini wa makubaliano hayo ulihudhuriwa rasmi na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, na ulionekana kuwa hatua muhimu ya kuimarisha juhudi za pamoja katika kukuza teknolojia safi za nishati na kuongeza ubadilishanaji wa maarifa ili kufanikisha malengo ya muda mrefu ya nishati nchini Tanzania.

Tukio hili lilifanyika sambamba na ushiriki wa TGDC katika Maonesho ya Osaka Expo 2025, ambapo kampuni hiyo ilifanikiwa kuwasilisha uwezo wa Tanzania katika sekta ya jotoardhi, pamoja na fursa zinazopatikana kwa wawekezaji wa kimataifa.



# Waziri Mkuu Aalika Wawekezaji wa Kijapani Kuchangamkia Fursa za Jotoardhi Nchini Tanzania

Timu ya TGDC ilifanikiwa kukutana na wadau kama Sumitomo Corporation, Toshiba, JOGMEC, Yokogawa Electric pamoja na JICA.

Mkutano huo na makubaliano yaliyofikiwa ni sehemu ya mkakati mpana wa Serikali ya Tanzania wa kuvutia uwekezaji wa kigeni na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Japan katika sekta ya nishati na maendeleo ya viwanda.

Kupitia makubaliano haya, TGDC na Toshiba wameonyesha dhamira ya pamoja ya kusukuma mbele maendeleo ya nishati ya jotoardhi, kuimarisha ushirikiano wa kiufundi, na kushirikiana katika tafiti, teknolojia na uwekezaji.












OSAKA,KANSAI,JAPAN
2025


WELCOME
EXPO




WELCOME
OSAKA,KANSAI,JAPAN
2025

OSAKA, JAPAN









**OSAKA, JAPAN**



# "LENGO NI KUIFANYA JOTOARDHI KUWA BIDHAA"

Eng. Mathew Mwangomba

Meneja Mkuu - TGDC




Mabalozi na Wawakilishi wa nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Watu wa Malawi, Mhe. Said Juma Mshana na Mhe. Agnes Kayola wamesema, ipo haja ya Watanzania ikiwemo Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) kutoka na kutembelea nchi wanazoziwakilisha kwa lengo la kuangalia fursa za Uwekezaji.

Wameyasema hayo kwa wakati mmoja walipopita katika banda la Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) Mei 27, 2025 wakati wa Maonesho ya Mbeya City Expo 2025 yaliyofanyika katika viwanja vya Uhindini mjini Mbeya yaliyoanza Mei 23, 2025 na kuhitimishwa Mei 31, 2025 yaliyoandaliwa na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania kwa mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya.

"ninawaalika Malawi, zipo fursa nyingi huenda utaalamu wenu ukatumika kama fursa hususan upande wa nishati, hivyo tokeni, msijifungie. Lakini pia ninawaalika wadau mbalimbali kuja kuwekeza katika miradi ya Jotoardhi hapa Tanzania kupitia TGDC", alisema Balozi Agnes Kayola

"ninawakaribisha mshiriki maonesho ya madini hivi karibuni, njooni mjifunze na mnyakue fursa mbalimbali na niungane na Mhe.Balozi Agnes kuwaalika wawekezaji kwenye sekta ya nishati ya jotoardhi", alimaliza Mhe. Balozi Said Mshana.




Katika hatua nyingine, Makamu Mkuu wa Chuo cha Kiislam Morogoro ambaye pia aliwahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) Prof. Mussa Assad alisema, "gharama ya kuanza utekelezaji miradi huwa kubwa, si kwa miradi ya jotoardhi pekee, ila tunachotazama ni muda wa kurejesha faida na jotoardhi ni ya muda wote, hivyo ukiwekeza unaweza kurudisha faida kwa muda wote wa maisha. Huu ni uwekezaji mzuri sana kuliko uwekezaji mwingine",

Prof. Assad alimaliza kwa kusema kuwa, "ningependa kuwaalika wawekezaji, hasa wa ndani ambao wanaweza kuwekeza kwenye Sekta ya jotoardhi"

TGDC ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) iliyoanzishwa mwaka 2013 na kuanza shughuli zake rasmi mwaka 2014 kwa lengo la kufanya tafiti na kuendeleza rasilimali ya jotoardhi Tanzania ili kuzalisha umeme.

# Mbeya City Expo 2025 Yaivuta TGDC Nje ya Mipaka ya Tanzania









# TGDC Yaonesha Ubunifu wa Nishati ya Jotoardhi Katika Wiki ya Nishati Jadidifu 2025

Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imeendelea kuonyesha dhamira yake ya kuchochea maendeleo ya nishati safi na endelevu kupitia ushiriki wake katika Wiki ya Nishati Jadidifu 2025, iliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 hadi 29 Mei 2025.

Wiki hii ya Nishati Jadidifu, imewaleta pamoja wadau mbalimbali wa sekta ya nishati kwa lengo la kuchambua njia bunifu za kuharakisha matumizi ya vyanzo vya nishati safi, uhakika na endelevu.

TGDC, kupitia Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, Mhandisi Shakiru Idrissa Kajugus, ilishiriki kikamilifu katika Kikao cha Nne: Kufungua Hazina ya Jotoardhi, ambapo aliwasilishga mada kuhusu matumizi ya nishati ya jotoardhi katika muktadha wa maendeleo ya Tanzania.

Katika uwasilishaji wake, Mhandisi Shakiru alieleza maeneo mbalimbali ya kimkakati yanayoweza kunufaika na jotoardhi, ikiwemo:

Uboreshaji wa ufanisi wa matumizi ya nishati kwa viwanda na watumiaji wakubwa wa umeme

Fursa za uwekezaji na utalii unaotegemea jotoardhi.

Mchango wa jotoardhi katika kilimo na usalama wa chakula.

Nafasi ya jotoardhi katika uchumi wa kijani na masoko ya mikopo ya kaboni (carbon credit)

Kikao hicho kilihitimishwa kwa kipindi cha maswali na majadiliano kilichoangazia nafasi ya jotoardhi kama kichocheo muhimu cha maendeleo endelevu na mageuzi ya kiuchumi nchini.

Aidha, Mhandisi Mkufu Tindi, Meneja wa Utafiti na Ubunifu TGDC, alipata heshima ya kushiriki katika Kikao cha Saba kilichojadili Usawa wa Kijinsia na Ubunifu wa Kidijitali katika Ufanisi wa Nishati kwa Wanawake na Vijana.




*"Jotoardhi si nishati tu ya umeme – ni fursa ya kiuchumi, kilimo endelevu, utalii wa kisasa, na suluhisho la kweli kwa mabadiliko ya tabianchi. Tunapoiendeleza, tunaiendeleza Tanzania yenye uchumi wa kijani."*

**Mha. Shakiru Idrissa Kajugus, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, TGDC**

**KIKAO CHA SABA**
kilichojadili Usawa wa Kijinsia na Ubunifu wa Kidijitali katika Ufanisi wa Nishati kwa Wanawake na Vijana. Katika mchango wake, alisisitiza umuhimu wa kuendeleza ubunifu jumuishi zinazowezesha upatikanaji wa nishati endelevu kwa makundi yote ya jamii.

Ushiriki wa TGDC katika Wiki ya Nishati Jadidifu 2025 ni ushahidi wa juhudi zake katika kuendeleza nishati ya jotoardhi kama mhimili sahihi wa nishati safi na utekelezaji wa malengo ya maendeleo Jotoardhi nchini Tanzania.










*"Wanawake wana nafasi ya kipekee katika mapinduzi ya nishati jadidifu, na jotoardhi ni jukwaa lenye nguvu la ubunifu, ajira, na mabadiliko ya kijamii. Tunatoa wito kwa wanawake wote kuja kuwekeza kwenye nishati hii endelevu kwa vizazi vyote."*

**— Mha. Mkufu Tindi, Meneja wa Utafiti na Ubunifu, TGDC**

# Idara ya Huduma za Ufundi Yafanya Kikao Kazi, Morogoro.

Dar es Salaam, Juni 20, 2025 — Timu ya Idara ya Huduma za Kiufundi kutoka Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imefanya kikao kazi maalum cha kujengeana uwezo na kuweka mikakati ya utekelezaji kuelekea hatua ya uchimbaji wa kisima cha kwanza cha uhakiki katika Mradi wa Jotoardhi Ngozi mkoani Mbeya.

Kikao kazi hicho kilifanyika kwa lengo la kuimarisha mshikamano, kuongeza ufanisi na kuratibu kwa pamoja shughuli zote muhimu za maandalizi ya mradi huo. Kikao hicho kiliendeshwa na Mkurugenzi wa Huduma za Kiufundi, Dkt. Keneth Lupogo, kwa kushirikiana na Meneja Mradi wa Ngozi, Mha. John Lubuva.


Katika kikao hicho, masuala mbalimbali yaliyoainishwa kama changamoto yalijadiliwa kwa kina na kupatiwa suluhisho, ikiwemo usimamizi wa vifaa, uratibu wa timu ya utekelezaji, na hatua za kiufundi zitakazochukuliwa kuhakikisha uchimbaji wa kisima cha uhakiki unatekelezwa kwa ubora na kwa wakati.

Katika hatua ya kujiimarisha zaidi kitaalamu, tarehe 14 Juni 2025, timu ya Idara ya Huduma za Kiufundi ya TGDC ilitembelea mradi wa kuzalisha umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere, mkoani Morogoro. Ziara hiyo ya mafunzo ilikuwa sehemu ya kupata uelewa wa kina kuhusu usimamizi wa miradi mikubwa ya nishati, na kujifunza mbinu bora za utekelezaji, usalama, na ushirikiano baina ya timu mbalimbali.

Mradi wa Jotoardhi wa Ngozi unatarajiwa kuwa mojawapo ya miradi mikubwa ya nishati jadidifu nchini, ukilenga kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.






TGDC, TUNA JAMBO LETU NGOZI...
KWA TAARIFA ZAIDI, KAA KARIBU NA MITANDAO YA KIJAMII

# Bonanza la Nishati Lafana Jijini Dodoma, TGDC Yashiriki



Dodoma, Juni 28, 2025 — Bonanza la Nishati 2025 limefanyika kwa mafanikio makubwa leo katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, likiwakutanisha watumishi kutoka taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Nishati kwa siku ya michezo, afya na mshikamano.

Bonanza hilo limefunguliwa rasmi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, aliyesisitiza umuhimu wa michezo kazini kama chachu ya afya bora, ushirikiano, na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma. Hafla hiyo pia imehudhuriwa pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.




Katika bonanza hilo, Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) ilionyesha ushiriki wa hali ya juu, ikiwa ni pamoja na kushiriki kwa mara ya kwanza katika mchezo wa mpira wa miguu. TGDC ilicheza mechi ya utangulizi dhidi ya TANESCO ambapo licha ya kushindwa kwa mabao 4–3, timu hiyo ilionyesha ushindani mkubwa na moyo wa kujituma.

Michezo mingine iliyoshirikisha taasisi mbalimbali ni pamoja na kufukuza kuku, bao, drafti, riadha, na rede ambapo wafanyakazi wa TGDC walishiriki kwa ari na hamasa kubwa. TGDC imefanikiwa kunyakua medali kwenye michezo kadhaa kama vile Riadha, Kukimbia kwenye gunia, kukimbia yai na kukimbia kwenye vikwazo, na pia kwenye kukimbiza kuku.

Bonanza hili limeendelea kuimarisha mshikamano baina ya taasisi za sekta ya nishati huku likihamasisha maadili ya kazi, afya ya mwili na akili, na kukuza utamaduni wa kushirikiana nje ya mazingira ya kazi ya kila siku.







# BONANZA LA NISHATI LAFANA JIJINI DODOMA, TGDC YASHINDA MEDALI 19



# Bonanza la Nishati Lafana Jijini Dodoma, TGDC Yashiriki












Tuzo
hii imetolewa kwa
TGDC
Kwa kushiriki katika Bonanza
la Nishati 2025
Tuzo
Hii imetolewa na Naibu
Waziri Mkuu na Waziri wa
Nishati Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko
NISHATI
BONANZA

# MEI MOSI 2025








Mkurugenzi wa Huduma za Kiufundi, Dkt Keneth Lupogo Akimkabidhi Mhandisi John Lubuva, Hati ya Pongezi kwa Kuwa Mshindi wa Jumla Sherehe za Mei Mosi









Mkurugenzi wa Huduma za Kiufundi, Dkt Keneth Lupogo Akimpongeza Mhandisi John Lubuva, na kumkabidhi zawadi zake kwa Kuwa Mshindi wa Jumla Sherehe za Mei Mosi

**Dar es Salaam & Mbeya – Mei 1, 2025** — Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) iliungana na wafanyakazi kote nchini kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), kwa kuandaa hafla maalum ya kuwapongeza na kuwazawadia wafanyakazi waliofanya vizuri.

Maadhimisho hayo yaliongozwa na Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Mathew Mwangomba, ambapo Bi. Rukia George alitangazwa kuwa mfanyakazi bora na mshindi wa jumla kwa mwaka 2025. Alipokea zawadi na cheti chake kama ishara ya kutambua mchango wake katika utendaji kazi.

Kwa upande wa ofisi ya Mbeya, Mhandisi John Lubuva alitunukiwa zawadi na cheti cha mfanyakazi bora, akipokea tuzo hiyo kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Kiufundi, Dkt. Keneth Lupogo.

Sherehe hizo ziliambatana na chakula cha pamoja na hotuba ya Meneja Mkuu, ambaye alisisitiza umuhimu wa kupendana, kushirikiana, na kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha jotoardhi inageuka kuwa bidhaa ya kweli kwa maendeleo ya taifa.












Meneja Mkuu wa TGDC Mha.Mathew Mwangomba (katikati) Akimkabidhi Rukia George, Zawadi yake kwa Kuwa Mshindi wa Jumla Sherehe za Mei Mosi




Meneja Mkuu wa TGDC Mha.Mathew Mwangomba Akimkabidhi Rukia George, Cheti chake kwa Kuwa Mshindi wa Jumla Sherehe za Mei Mosi




**TGDC**

Nyumba Na. 25 Ursino,
Barabara ya Mwai Kibaki
P.O Box: 14801 Dar es Salaam
Phone No: +255 687 833 855
Email: info@tanesco.co.tz
**www.tgdc.go.tz**